HOTUBA YA MHESHIMIWA MAMA SALMA KIKWETE WAKATI WA UZINDUZI WA KIKUNDI CHA VICOBA DEBORA KATIKA UKUMBI WA NEXT DOOR SEGEREA TAREHE 26/06/2010, SAA 5.00 ASUBUHI

Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa

Mwakilishi wa Meya wa Jiji la Dar es Salaam,

Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilala,

Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya Ilala, Bwana Leonidas Gama,

Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Ukonga, Bwana Makongoro Mahanga,

Mwenyekiti wa UWT Mkoa, Bibi Zarina Madadiba,

Waheshimiwa Wakuu wa Taasisi za fedha (Twiga Benki na Benki zote zilizopo hapa),

Mwenyekiti wa Kikundi cha VICOBA cha DEBORA, Bibi Magreth Shauri,

Mheshimiwa Diwani wa Kata ya Tabata Bibi Grace Stanley,

Viongozi wote wa Vyama na Serikali,

Wawezeshaji wa mpango wa VICOBA Asasi ya UYACODE,

Viongozi wa Taasisi na Mashirika mbalimbali,

Wanachama wa VICOBA toka sehemu mbalimbali,

Wana VICOBA DEBORA,

Waandishi wa habari,

Mabibi na Mabwana.

Naomba nianze kwa kumshukuru mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema. Pia nichukue fursa hii kuwashukuru viongozi na wanachama wa kikundi cha VICOBA CHA DEBORA kunialika mimi kama Mwenyekiti wa WAMA kuwa Mgeni Rasmi katika shughuli hii ya uzinduzi wa kikundi cha VICOBA cha DEBORA.

Pia nitumie fursa hii kuwapongeza kwa kuwaalika wanachama wengine wa mpango huu wa VICOBA waliotoka sehemu mbalimbali za wilaya hii na pia Mikoa ya jirani ya Tanga, Kilimanjaro na Pwani. Pamoja na wafanyabiashara wadogo

na wakubwa wanaowazunguka hapa kwenu segerea na Jiji zima. Huu ni ubunifu unaostahili kuigwa kwani kushiriki kwao ni moja ya juhudi zenu za kuunda umoja na ushirikiano katika suala zima la kuikwamua jamii ya kipato cha chini. Mmeweza kufanya hivyo kwa kushirikishana katika shughuli mbalimbali za uzalishaji mali, kutafuta masoko na utunzaji wa Akiba.

Ndugu wananchi,

Kwa namna ya pekee nichukue nafasi hii kwa niaba ya WAMA kuwapongeza Asasi ya UYACODE waliowezesha mafunzo ya mpango huu hapa Dar es Salaam na kwingineko Tanzania Bara na kuwataka waendelee kuwasaidia wanajamii wengine wa kipato cha chini ili waweze kujianzishia mitaji yao wenyewe . Lakini kubwa zaidi ambalo ndio msingi wa VICOBA ni utaratibu na kanuni za uanzishaji na usimamizi wa vikundi vya kijamii somo ambalo ndilo linaloonyesha Dira ya muelekeo wa wanachama.

Nichukue pia nafasi hii kuwashukuru sana wenzetu wa Benki ya TWIGA ambao wameamua kwa dhati kushirikiana na vikundi hivi vya VICOBA na kuweza kuwakopesha basi; Benki

hii inastahili pongezi kubwa!. Kazi kubwa iliyo mbele yenu wana VICOBA ni kusimamia kwa uhakika mradi huu na kufanya vizuri; ili muweze kujenga imani kwa taasisi za fedha kuwa vikundi hivi vinakopesheka.

Aidha niwapongeze sana wanachama wote wa VICOBA DEBORA mliopata nafasi hii ya kuhudhuria mafunzo haya, kadhalika niwakumbushe wana VICOBA wengine mliotoka sehemu mbalimbali kuwa mtumie muda huu wa siku ya leo kujikumbusha yale mliyofundishwa awali ili muweze kuendeleza vikundi vyenu kwa kufuata mafunzo bora mliyojifunza kwa lengo la kufikia malengo mliyokusudia.

Ndugu Mwenyekiti,

Katika risala yenu, mmeeleza kuwa ili jamii ijinasue kutoka katika umaskini, inahitaji kuwa na utaratibu mzuri na sio fedha pekee. Nimefarijika kufahamu kuwa katika mpango wa VICOBA, suala la *FEDHA* na *UTARATIBU* vinapatikana humo. Hii ni ishara njema inayoleta matumaini kwa jamii. Kwani ni dhahiri kuwa mtu asiye na malengo hastahili kupewa fedha,

kwa sababu fedha bila utaratibu ni sawa na mali bila daftari, ambayo hupotea bila habari.

Pia napenda mtambue kuwa Serikali inathamini mchango wa asasi zinazotekeleza mipango ya Serikali ya kuwawezesha wananchi kushiriki katika shughuli za vikundi zinazolenga katika kujikwamua kiuchumi. Ninyi ni kati ya asasi zinazofanya kazi nzuri, kwani siku ya leo ni ushahidi wa kutosha unaodhirisha kazi kubwa mnayoifanya. Aidha, nitumie fursa hii kuwaasa wana VICOBA wote, kutumia vizuri fursa zilizopo kwa ajili ya Maendeleo ya jamii.

Ndugu wananchi,

Nimetembelea na kuona bidhaa mnazozalisha ambazo ni nzuri sana na nimeweza kutambua kuwa jamii ikiwezeshwa inaweza kufanya mambo mazuri sana. Hongereni sana! Lakini napenda kuwakumbusha kuwa uzalishaji huu wa bidhaa, ingefaa uendane na upatikanaji wa soko la uhakika. Hii itawahakikishia kipato na kukua kwa biashara zenu. Ili haya yafanikiwe, mnahitaji kuzingatia ubora wa bidhaa zenu

na pia kuwa wabunifu na hivyo kuongeza ukubwa wa masoko ya bidhaa hizo.

Hata hivyo, ni vyema watengenezaji wa bidhaa hizi kuzingatia viwango kwa kufuata ushauri wa kitaalam. Zipo asasi mbalimbali ambazo hutoa maelekezo katika utayarishaji wa bidhaa, ufungashaji na kutoa taarifa za masoko. Asasi hizo ni pamoja na SIDO, na Chama cha wasindikaji wa vyakula (TAFOPA). Pia mjitokeze kutembelea katika maonesho mbalimbali ya bidhaa kama vile maonesho ya kimataifa ya Saba Saba ambako mnaweza kujifunza mengi na kupata taarifa za masoko na watoa huduma.

Ndugu Wananchi,

Dira yenu ya kutaka kuwa chombo cha uwekezeshaji au Asasi ya fedha ni nzuri sana, pamoja na kwamba ina changamoto nyingi lakini ni mawazo endelevu yanayotakiwa kuwekwa kitaalamu ili kuepusha aina yoyote ya mashaka kwani masuala ya fedha yanahitaji umakini ili yasiweze kupoteza imani ya wanachama. Kwani kila mtu anahitaji kuwa na fedha, lakini jambo la msingi ni kuandaa utaratibu mzuri

ambao utawawezesha kupata fedha na kuzirejesha kwa utaratibu uliopangwa. Ndio maana nasisitiza kuwa suala hili linahitaji umakini wa hali ya juu ambao sina shaka ninyi wana VICOBA mnautambua vizuri.

Pia ningependa kuwakumbusha kuwa Serikali imeandaa mipango na mikakati ya kuwasaidia wananchi ili waweze kujikwamua kiuchumi. Lakini hili, linaweza kufanikiwa vizuri sana kwa kujiunga katika vikundi vya kiuchumi kama ambavyo ninyi mmefanya. Kwa hiyo, wale wote ambao hawajajiunga katika vikundi hivi, muwahimize wajiunge ili Serikali iweze kuwasaidia vizuri. Kwani Serikali kupitia Manispaa za Wilaya, ina utaratibu mzuri wa kusimamia utoaji wa pesa kwa vikundi kupitia mifuko maalum kama ule unaojulikana kwa jina maarufu la mfuko wa JK. Hivyo umoja huu uwe chachu ya kuwavuta wengine kujiunga na kuweza kupata mafanikio mliyoyapata ninyi. Kwa kuwa viongozi wa Mkoa na Wilaya wote tunao hapa nina imani kuwa, viongozi hawa watawasaidia pale inapobidi kufanya hivyo kwani jitihada zenu zinaonekana.

Ndugu wana VICOBA,

Katika risala yenu mmeeleza juu ya ndoto yenu ya kutaka kuwa wawezeshaji kwenye jamii hasa inayowazunguka (wakopeshaji), kuingia kwenye mradi wa kilimo ili kutekeleza azimio la kilimo kwanza, uchimbaji wa madini na kujenga hosteli ya wasichana . Haya ni mawazo mazuri yanayoonyesha ari mliyonayo katika kujikwamua kiuchumi na kuleta Maendeleo kwa nchi yetu. Nina imani na usemi usemao kuwa, "Penye nia pana njia" hivyo kwa jitahada za dhati nina amini mtafanikiwa.

Katika risala hiyo pia, mmeomba mambo mbali mbali ikiwa ni pamoja na kutaka kuunganishwa na fursa mbali mbali za kimaendeleo zilizopo. Mimi nikiwa kama Mwenyekiti wa Taasisi ya WAMA, kwa niaba yangu na wafanyakazi wote kwa ujumla tuko tayari kushirikiana nanyi katika mambo yaliyo ndani ya uwezo wetu ikiwa ni pamoja na kuwaunganisha katika fursa hizo zilizopo pale tunapoweza kufanya hivyo. Jambo kubwa ni mawasiliano ya karibu

Ndugu Wananchi

Naomba nimalizie kwa kuwapongeza kwa kuanzisha umoja wenye maendeleo na pia kujiwekea akiba ambayo imewawezesha kuwa na mitaji yenu. Pia nashauri kutumia fursa ya mafunzo ili muweze kufanikiwa zaidi.

Baada ya kusema hayo natamka rasmi kuwa, "Kikundi cha DEBORA VICOBA sasa KIMEZINDULIWA!

AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA!